REVIVAL NEWS
From **Revival Ministries Australia**
P.O. Box 2718 BC TOOWOOMBA Q4350 Australia
Phone: 61-7-46130633; e-mail: rma@revivalministries.org.au
Website: www.revivalministries.org.au

****** DISEMBA 2020 **** DISEMBA 2020 **** DISEMBA ******

UFUFIO KIDOGO

Baadhi ya ahadi za Mungu kwetu kutoka kwa Kitabu cha Ezra

"Na sasa kwa muda kidogo tumeneemeshwa na Bwana, Mungu wetu, hata akatuachia mabaki yaokoke, akatupa msumari katika mahali pake patakatifu. Mungu wetu atutie nuru machoni mwetu, tuburudike kidogo katika kufungwa kwetu. Maana sisi tu watumwa; lakini Mungu wetu hakutuacha katika utumwa wetu, bali ametufikilizia rehema zake, mbele ya wafalme wa Uajemi, ili kutuburudisha, kusimamisha nyumba ya Mungu wetu, na kuitengeneza palipobomoka , atupe ukuta katika Yuda na Yerusalemu" **Ezra 9:8-9.**

Ni ajabu kufikiri kwamba ombi la Ezra la takriba miaka 2500 iliyopita linajibiwa sasa. Misitari miwili hii ya Andiko ilikuja katika masomo yetu ya kila siku majuma machache yaliyopita [wengi wetu husoma Maandiko kila siku, kufuatilia mpangilio ambao hutuwezesha kusoma Bibilia nzima kwa mwaka mmoja]. Ilionekana hatukuwa tumeona ombi la ***"ufufio kidogo",*** lakini kwa ghafla ilikuwa hapo na Mungu alikuwa ananena kupitia misitari hii.

Jinsi gani tumetamani ufufio kidogo! Tumeangalia 'ufufio' zilizopita ambazo tumehusika nazo na tumekuwa tukiombea ufufio uje tena, lakini kwa furaha tunamwambia 'sio kama ufufio ambazo zimepita' bali ufufio, wakati ***"wa kuburudika"*** **(Matendo 3:19),** ambao utuingiza katika lengo la Mungu katika wakati wetu [siku ambazo tunaishi ndani].

Kila kitu kwa neema

Kitu cha kwanza tunahitaji na tunategemea sana ni neema ya Mungu. Tumeipitia hiyo neema tangu Mungu alipotuleta kwanza kwa wokovu katika Yesu Kristo (**Waefeso 2:8),** na neema kubwa iliyoachiliwa ambayo tulipitia wakati Mungu alipotuleta kwa ***"kutuchagua ili tufanywe wanawe kwa njia ya Yesu Kristo"*** **(Waef.1:5).** Hii imekuwa kwa ***"kusifiwa kwa utukufu wa neema yake"*** **(Waef.1:6).** Hii ilianza kwa msimu wa ajabu katika 2002, na katika miaka iliyofuata tulihudumu neema ya kufanywa wana **(Warumi 8:15, Wagalatia 4:5)** kwa ndugu wengi katika mataifa mengi.

Mabaki yataokoka

Neno la Mungu linarejelea 'mabaki' na muhimu sana kutambua ahadi za kuhusu masazo. Paulo, akinukuu kutoka kwa Isaya anasema, ***"ijapokuwa ni kama mchanga wa bahari, ni mabaki yao tu watakaookolewa"*** **(Warumi 8:27).** Paulo anajitambua kama sehemu ya mabaki ya Waisraeli ambao wanaokolewa katika Masiha Yesu (**Warumu 11:1).** Paulo kisha anarejelea mabaki ya ***"watu elfu saba wasiopiga goti mbele ya Baali"*** **(mst.4)** katika siku za Eliya. Paulo kisha anasema ***"wakati huu sasa, yako mabaki waliochaguliwa kwa neema"*** **(Warumi 11:5).** Mabaki hayo ni

kama ***"watu wake mwenyewe wa kipekee"*** au ***"mzao mteule"*** **KJV(1Pet.2:9).** Kuokoka ni kwenye Mahali Pake Patakatifu**(Ezra 9:8).**

Msumari katika Mahali Pake Patakatifu

Tazama kwamba msumari wa hema iko katika Mahali Patakatifu, sio sehemu ya nje. Katika sehemu ya nje kuna kila aina ya mafundisho na imani ambazo zitatufunga lakini tunapofungwa katika Mahali Patakatifu **(Waebrania 6:19-20),** hatuwezi kutingizika.

Yafuatayo yalionekana kwenye Facebook kutoka kwa nabii Joshua Otieno wa Kenya Magharibi:

> MSUMARI WA HEMA- ***"Kwake yeye utatoka msumari"*** **(Zakaria 4:10).** Huu msitari pia unarejelea 'jiwe la pembeni' kutokea, ambalo kwa hakika ni Yesu aliye Masihi.
> Kutoka kwa nyumba ya Yuda, Yahweh aliahidi kwamba kutatokea, MSUMARI WA HEMA. Nakili za Bibilia zingine humwita *"msumari wa ukuta",* au *"msumari".* Hii ni ahadi ya kinabii ya kuja kwa Masiha Yesu kwa kuwa ***"Amekuwa kabla ya vitu vyote, na vitu vyote hushikana katika yeye"*** **(Wakolosai 1:17).** Masiha Yesu ndiye msumari wa hema wa kanisa lake, nyumba yake, mwili wake, kwa kuwa ***"Vyote vilifanywa kwa huyo ; wala pasipo yeye hakikufanyika cho chote kilichofanyika"*** **(Yohana 1:3).**
> O jinsi gani uhakikisho na faraja kwa wale ambao wanashikana pamoja naye hazielezeki; hawataishi kwa woga wala kufanya haraka, kwa kuwa ***"Ni msingi ulio imara; yeye Mungu aaminiye hatafanya haraka"*** **(Mathayo 28:16).**
> Milango ya kuzimu haitaweza kamwe, kufaulu dhidi ya "Msumari wa hema" **(Mathayo 16:18).** Ni muhimu jinsi gani kila mara imani yetu na ujasiri iko katika Masiha Yesu ,na sio kwa binadamu wa kufa ambaye ana kivuli cha kubadilika. "Misumari mingine ya hema" inapobadilika na kuleta masikitiko makubwa, na matarajio yetu yanasambaratika mbele ya macho yetu, kuna mwito wa kimbinguni kila mara na kukumbushwa kwamba Mungu amemfanya huyo Yesu, ***"mliyemsulubisha kuwa Bwana na Masiha"*** **(Matendo 2:36).**

Angaza macho yetu

Paulo anaomba ya kwamba Mungu aweze ***"kutia nuru macho ya mioyo yetu"*** **(Waef.1:18).**Yesu alisema kwamba tunahitaji mafuta ya macho kupaka macho yetu ***"ili tuweze kuona"*** **(Ufunuo 3:18).** Mungu alimwuliza Yeremia ***"Waona nini?"*** **Yer.1:11&13).** Yeremia alijua kuona katika roho. Yesu alipomega mkate na wanafunzi Emau "***Yakafumbuliwa macho yao, wakamtambua"*** **(Lk.24:31).** Kutiwa nuru macho yetu nikupata ufunuo **(Waef.1:17).**

Ufufio Kidogo

Nakala ya King James inafasiri ***"ufufio kidogo"*** kama ***"kuburudishwa kidogo"*****(Ezra 9:8).** 'Ufufio Kidogo' inakaa aje? 'kuburudishwa kidogo' ni nini? Je, unatambua kwamba kuburudishwa kidogo kutoka kwa Mungu ni kubwa sana katika macho yetu?Wengi huota juu ya ufufio mkubwa kuja kwa nchi yetu, miji mizima kumgeukia Mungu! Mwana ufufio mashuhuri kuja kuhubiri! Lakini kile tunahitaji ni 'kuburudishwa kidogo', 'wakati wa kuburudishwa' **(Matendo 3:19),**

- Ambapo Mungu anajaza maisha yetu na neema yake na tunajua kwamba ***"tu kazi yake, tuliumbwa katika kristo Yesu, tutende matendo mema, ambayo tokea awali Mungu aliyatengeneza ili tuenende nayo"*** **(Waef.2:10).**

- Ambapo Mungu huhuisha ndani yetu tamaa ya kumtafuta, kupitia neema yake na mwongozo wake [kusikia sauti yake] ,kujua upya uguzo wa upako wake ambao huvunja nira ya mtesi **(Isa.10:27),** ambao huwezesha mwenye nguvu wa shetani kufungwa **(Mathayo 12:29),** na kuwafungua waliofungwa kutembea katika makusudio waliopewa na Mungu.
- Na huu ni ukristo wa kawaida, kuburudishwa kidogo kutoka kwa Mungu ambao unatuwezesha kutembea na kunena na kuishi maisha hiyo kila siku. Tunapopokea kipimo cha ufufio, tunampitia Mungu, tunasikia sauti yake na tunakuwa na shuhuda za kushiriki. Hii imekuwa ikitufanyikia kati yetu katika njia za ajabu katika wiki za majuzi, na milango mipya imekuwa ikifunguka kwa watu binafsi na kwa huduma ya RMA, nchini na dunia nzima.

Maana ya maneno

'kidogo'-SC Kihibrania #4241: inamaanisha kirahisi *kidogo au chache; NKJV inafasiri hilo neno kama 'kiasi'*

'kuburudisha'-SC Kihihrania #4592: inamaanisha *kuburudisha, kuhifadhiwa kwa maisha, uhimilivu, yaani, waliohai.* Neno 'hai' hutokea katika nakala ya King James, lakini kwa kuwa ni neno la zamani la Kiingereza, si nyingi katika Kingereza leo, lakini ni neno la nguvu. Kwa mfano, KJV **Waebrania 4:12** ***"neno la Mungu li hai, tena lina nguvu";*** **Warumi 8:11** ***"Roho…atahuisha na miili yenu iliyo katika hali ya kufa",*** na marejeleo mengine ya ajabu katika KJV kwa neno 'hai' na 'kuhuisha', iliyofasiriwa katika NKJV kama 'ufufio'.

Tulikuwa watumwa

"Maana sisi tulikuwa watumwa; lakini Mungu wetu hakutuacha katika utumwa wetu, bali amutufikilizia rehema zake" [katika muktadha huo watu wa Mungu walikuwa katika utumwa kwa wafalme wa Uajemi] **(Ezra 9:9a).** Katika **msitari 8,** Ezra alirejelea neema ambayo Mungu alionyesha na sasa anarejelea rehema ya Mungu, kutuhuisha, hata katika utumwa wetu, kufanya kazi ya Mungu ambayo inahusu nyumba ya Mungu. **Waebrania 4:16** inaleta neema na rehema pamoja katika kiti cha enzi chenyewe cha Mungu.

Matokeo ya 'kuburudishwa kidogo'

Ezra anaomba kwa kipimo cha ufufio, kuburudishwa kidogo ili:

- Kurekebisha nyumba ya Mungu [KJV 'kusimamisha nyumba ya Mungu wetu']
- Kujenga upya magofu yake [KJV 'kurekebisha magofu yake']
- Kutupa ukuta katika Yuda na Yerusalemu.

Kurekebisha nyumba ya Mungu

Katika siku yetu, kanisa la Yesu Kristo linahitaji urekebisho wa kumaanisha. Lile ambalo linaitwa kanisa hasa halijajengwa kuambatana na kiolezo cha Maandiko. Ili kanisa la kweli litokelezee katika enzi yetu kunahitajika kuwa na **kung'oa, kubomoa, kuharibu na kuangamiza,** kabla ya kuwa na **kujenga na kupanda (Yer.1:10).** Mengi ya kanisa linafuata mafundisho, imani, na matendo ya kidini [iliyoundwa na binadamu]. Makanisa machache sana yamejengwa juu ya msingi wa Kibibilia (**1 Kor.3:11; Waefeso 2:20).**

Kunahitajika kuwa na kutambua na kupokea karama tano za huduma ambazo zimepeanwa na Kristo wakati wa kupaa kwake **(Waefeso 4:7-8)** na huduma tano za mtume, nabii, muinjilisti,

mchungaji, na mwalimu lazima wafanye ***"kazi ya huduma"*** hadi kanisa lote ***"lifikie umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu, hata kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo"*** **(Waef.4:11-13).** Huu ndio urekebisho, au kuinua nyumba ya Mungu.

Tunahitaji zaidi ya wachungaji. Kila sehemu ya mwili inahitaji kuwa na ushirikiano na wahudumu wote wa huduma tano, ili kazi ya ujenzi uende mbele.

Kujenga upya magofu

Magofu yananena juu ya mjengo kwamba uliharibiwa. Haidhanii kwamba misingi ilikuwa imeharibiwa, bali misingi inahitaji kushugulikiwa, kurudisha kanisa kithabiti kuwekwa kwenye msingi ulio sawa, ***"Maana msingi mwingine hakuna mtu awezaye kuuweka, isipokuwa ni ule uliokwisha kuwekwa ,yaani, Yesu Kristo"*** **(1 Kor.3:11).** Habari ya mafundisho na mahubiri yetu yote, inapaswa kuwa ***"Yesu aliye Kristo"*** **(Matendo 5:42).** Yesu alisema atalijenga kanisa juu ya 'mwamba' wa ufunuo wa Yule aliye **(Mat.16:18).** Petro alikuwa amepokea ufunuo kwamba Yesu ndiye ***"Kristo Mwana wa Mungu Aliye Hai"*** **(Mat.16:16).**

Andiko linasema kuwa nyumba ya Mungu litajengwa ***"juu ya msingi wa mitume na manabii"*** **(Waefeso 2:20).** Haya siyo marejeleo kwa manabii wa Agano la Kale, bali marejeleo kwa manabii wa Agano Jipya **(Waef.3:5).** Mitume na manabii wote ni muhimu sana kuleta ufunuo wa kimsingi wa siri ya Kristo kwa watakatifu, ili kanisa liweze kujengwa kulingana na kiolezo, na watakatifu waweze kuja kwa ufahamu uliokomaa wa siri (**1Kor.2:6-8).**

Mwandishi kwa Waebrania anaangaza nuru kwa shida ya kutokomaa ambayo hutokea kwa kanuni za kimsingi ya neno la Mungu kukosa kuwekwa vizuri **(Waebrania 5:12-13).** Watakatifu walikuwa watoto wachanga kwa sababu misingi kukosa kuwekwa. Ilhali duniani nzima, sio watu wa kanisa pekee, bali wahudumu hawajui kabisa kanuni sita za kimsingi iliyowekwa katika **Waebrania 6:1-2.** Hatutapata ruhusa ya kuendelea kwa ukomavu kama misingi haipo mahali payo.

Lazima tujenge upya magofu ya nyumba ya Mungu!

Tupe ukuta

Neno la Kihibrania kwa 'ukuta' linasisimua sana. Linafasiriwa kama *ukuta, ua wa miti iliyomeeshwa, ua;* neno hilo linamaanisha *mzunguko* [hatukuwa tumewahi kusikia juu ya hili neno mbeleni], yaani, *kuzungusha kitu kwa ukuta; kufanya mzunguko, mahali salama; kulinda mji kwa kujenga ukuta.*

Mungu anataka tuishi ndani ya ukuta wa ulinzi, ambao huzuia adui nje na kutupa mahali salama pa kuishi ndani. Nehemia alitumwa kujenga ukuta kuzunguka mji wa Yerusalemu. Ni kazi alipewa na Mungu na tafadhali soma **kitabu cha Nehemia** kushika maono ya hitaji la kujenga ukuta huu. Tunahitaji kushirikiana na Mungu: Atatupa ukuta, lakini sisi ndio tunafaa kuujenga, na lazima tusikubali adui kuingia katikati ya wafanyi kazi wetu kuzuia au kusimamisha kazi.

Mungu mwenyewe analalamikia ukosefu wa ukuta. Alisema ***"nikamtafuta mtu miongoni mwao, atakayelitengeneza boma, mahali palipobomoka ,kwa ajili ya nchi, nisije nikaiharibu, lakini sikuona mtu"*** **(Ezekieli 22:3).**

Bwana tujalie kipimo cha ufufio, kuburudishwa kidogo tu kutuwezesha
Kurekebisha nyumba ya Mungu, kujenga upya magofu yake
Na kutupa ukuta katika Mji wako Mtakatifu.

PAUL GALLIGAN.